# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

# TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA TATU (JANUARI-MACHI) TAREHE 30/04/2020 MWAKA WA FEDHA 2019/2020


*Imeandaliwa na Ofisi ya Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Manispaa,*
*S.L.P. 735*
*Simu: +255 736 200 910*
*Nukushi: +255 736 200 910*
*Simu: +255 736 200 911/912*
*Barua pepe md@ilemelac.go.tz*
*Tovuti www.ilemelamc.go.tz*


**Mwanza – Tanzania**

**Aprili, 2020**

Scanned by CamScanner

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA**

*Mhe. Mwenyekiti,*

*Wahe. Wajumbe,*

*Baraza la Madiwani,*

*Halmashauri ya Manispaa*

***ILEMELA.***

**YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA TATU (JANUARI – MACHI) TAREHE 30/04/2020 MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

## 1.0. UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti***, Kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani juu ya matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha kila robo ya mwaka.

***Hivyo taarifa hii itakuwa na mambo yafuatayo:-***

i. *Taarifa ya Ujio wa Ugeni wa Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI;*
ii. *Taarifa ya Utoaji wa Hati Milki za Ardhi kwa Wananchi na kuanza kwa safari ya Kivuko kipya cha MV. ILEMELA katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela;*
iii. *Taarifa ya Hati Safi;*
iv. *Taarifa ya Ugeni wa Kamati ya Bunge Ardhi, Maliasili na Utalii;*



Scanned by CamScanner

v. *Taarifa ya uwasilisahaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 katika OR-TAMISEMI, Hazina na Kamati ya Bunge ya Bajeti;*
vi. *Taarifa ya Mkakati wa kufundisha wanafunzi wa sekondari kwa njia ya Mtandao;*
vii. *Taarifa Juu ya tahadhari ya Ugonjwa unaotokana na Virus vya Corona (COVID -19);*

## 2.0. UFAFANUZI WA TAARIFA

### *2.1.1. Taarifa ya Ujio wa Ugeni wa Naibu wa Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI*

***Mhe. Mwenyekiti,*** mnamo tarehe 27/02/2020 Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Josephat Kandege alitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela na kukagua shughuli mbalimbali za Miradi ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na; ujenzi wa stendi ya mabasi na maegesho ya malori Nyamhongolo, ujenzi wa vyumba vya madarasa, ujenzi wa mradi wa mizani kwa ajili ya kupimia mazao ya samaki, ujenzi wa barabara Sabasaba-Kiseke-Buswelu na kutembelea shule ya Sekondari Buswelu na kufanya ukaguzi ujenzi wa madarasa na bweni kwa ajili ya kidato cha tano.

Vilevile, Mhe. Naibu Waziri alitembelea kikundi cha wanawake cha Amani Kilimahewa na kutoa agizo la kupewa Tshs. 20,000,000/= kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kiuchumi zitakazowaongezea kipato. Hata hivyo, utekelezaji wa agizo hili ulifanyika mnamo tarehe 24/03/2020 ambapo Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ilitoa kiasi tajwa hapo juu.



Scanned by CamScanner

Aidha, Mhe. Naibu Waziri aliipongeza Halmashauri kwa ushirikiano wao kuanzia ngazi ya jamii hadi uongozi wa juu wa Halmashauri.

### 2.1.2. *Taarifa ya Utoaji wa Hati Milki za Ardhi kwa Wananchi na kuanza kwa safari ya Kivuko kipya cha MV. ILEMELA katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.*

***Mhe. Mwenyekiti,*** *Mbunge wa jimbo la Ilemela ambaye pia ni* Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mhe. Dkt Angelina Mabula mnamo tarehe 07/04/2020 aliwezesha utoaji wa Hati Miliki za Ardhi 1,508 kwa wananchi wa Manispaa na kutoa shukrani na pongezi kwa uongozi na watumishi kwa jitihada zinazofanywa katika kumkomboa mwananchi kiuchumi. Hata hivyo, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela imekuwa ni mfano wa kuigwa kwa Halmashauri zingine nchini kwa kufanya vizuri katika zoezi la urasimishaji wa Ardhi na Makazi.

Vilevile tarehe 19/04/2020 Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Jimbo la Ilemela alihudhuria hafla ya kuanza kwa safari ya Kivuko cha MV ILEMELA kati ya Kayenze na kisiwa cha Bezi. Pia alimshukuru Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutoa kiasi cha Tshs. bilioni 2.7 ikiwa ni gharama ya utengenezaji wa kivuko hicho. Aidha, aliwasihi wananchi kukitunza na kukitumia kwa ufasaha kwa ajili ya kukuza uchumi wao. Pamoja na hayo, aliwaangiza wataalam wa afya kutoa elimu juu ya ugonjwa wa corona kabla na baada ya kuanza safari hapo kivukoni.



Scanned by CamScanner

### 2.1.3. *Taarifa ya Hati Safi*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Kwa mara nyingine Halmashauri yetu imekuwa ni miongoni mwa Halmashauri nchini ambazo zimepata Hati Safi. Hii ikiwa ni mara ya 6 mfululizo kwa kipindi cha miaka 6. Taarifa hii inatokana na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali iliyowasilishwa kwa Mhe. Rais wa Jumhuri ya Muungano Dkt. John Pombe Magufuli na baadaye kuwasilishwa kwenye Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mafanikio haya yanatokana na usimamizi na ushauri mzuri unaotolewa na Baraza lako.

### 2.1.4. *Taarifa ya Ugeni wa Kamati ya Bunge Ardhi Maliasili na Utalii*

***Mhe. Mwenyekiti,*** mnamo tarehe 16/03/2020 Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ilitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela ikiwa ni Halmashauri pekee iliyofanya vizuri katika mradi wa upimaji viwanja eneo la East Buswelu.

Vilevile Waheshimiwa Wabunge walifurahishwa na kupongeza utekelezaji wa mradi huo kwani umeleta tija kwa wananchi na kwa Serikali pia, ukizingatia kwamba deni la Tshs. 1,550,000,000/= ambalo lilikopwa kwa ajili ya mradi huo tayari limerejeshwa kwa muda muafaka katika Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Hata hivyo, Wajumbe wa Kamati walishauri kwamba uandaliwe Mpango Maalumu wa kuendeleza eneo hilo pengine Halmashauri ikishirikiana na mashirika ya umma kama Shirika la Nyumba Taifa (NHC), Watumishi Housing na mengineyo na kuona namna bora ya kuendeleza eneo hilo kwa kuzingatia mpango ulioandaliwa.



Scanned by CamScanner

### 2.1.5. *Taarifa ya Uwasilishaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 Katika OR-TAMISEMI, HAZINA na Kamati ya Bunge ya bajeti.*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Napenda kuritaafu Baraza lako kuwa mnamo tarehe 28/02/2020 Halmashauri yako iliwasilisha Rasmu ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2020/2021 katika OR –TAMISEMI na Hazina. Kwa ujumla kitabu kilipokelewa na kupongezwa kwa undaaji mzuri uliozingatia mambo muhimu yaliyoelekezwa katika Kitabu cha Mwongozo wa mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021. Vilevile, tarehe 26/03/2020 Halmashauri kupitia Mkoa iliwasilisha Randama ya Bajeti kwenye Kamati ya Bunge na kupokelewa. Kamati pia ilitoa pongezi kwa Halmashauri na Mkoa kwa ujumla kwa kuzingatia upelekaji wa fedha wa asilimia 10 za Mfuko wa Wanawake, Vijana na Walemavu. Hadi sasa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kuanzia mwezi Julai hadi Machi 31, 2020 imetoa jumla ya Tshs. 540,000,000/= kati ya Tshs. 835,604,700 ambayo ni sawa na 64% ya fedha yote. Jumla ya vikundi 126 vya wanawake vyenye watu 1,890 vilipokea Tshs. 418,000,000/=. Vikundi 32 vya vijana vyenye watu 480 vilipokea kiasi cha Tshs. 101,000,000 na vikundi 8 vya walemavu vyenye watu 40 vilipokea kiasi cha Tshs. 21,000,000/= kati ya fedha hizo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, ninaomba tuendelee kuhakikisha fedha hizi zinasimamiwa ili kufanikisha lengo husika kwa ajili ya wajasiriamali wadogowadogo ili kuwajengea uchumi na kuinua vipato vyao. Kwa sasa kazi zinazoendelea ni ukamilishaji wa bajeti kwa kuzingatia ukomo uliotolewa.



Scanned by CamScanner

### 2.1.6. *Taarifa ya Mkakati wa kufundisha wanafunzi wa sekondari kwa njia ya Mtandao*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Halmashauri yetu imeandaa Program ya kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa njia ya mtandao. Hivyo, Halmashauri inasisitiza wazazi kuwezesha wanafunzi kupata maswali kupitia simu zao. Pamoja na hayo, wazazi wanasisitizwa kuwasimamia wanafunzi kufuatilia vipindi mbalimbali vinavyotolewa kwa njia ya luninga na redio. Vituo hivyo ni pamoja na EA TV, Chanel TEN, RFA, KISS FM na Jembe FM kuanzia saa 4.00 asubuhi. Aidha, wito unatolewa kwa viongozi ngazi ya Mtaa na Kata wawasisitize wazazi kusimamia watoto wao kubaki majumbani katika kipindi hiki cha ugonjwa unatokana na virus vya corona.

### 2.1.7. *Taarifa Juu ya Tahadhari ya Ugonjwa unaotokana na Virus vya Corona (COVID 19)*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Kutokana na kuwepo kwa Ugonjwa unaosababishwa na virusi cha Corona (Covid 19), Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela inaendelea kuwasisitiza na kuwahimiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari kama zinavyoelekezwa na Wataalamu wa Afya dhidi ya ugonjwa huo.

Vilevile, hatua mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa na halmashauri kwa kuwaelimisha wananchi kupitia vyombo vya habari, magari ya matangazo na kuwatembelea katika maeneo yenye muingiliano mkubwa wa watu kama vile stendi ya mabasi Buzuruga na maeneo ya masoko.

Aidha, kuongeza nguvu ya utoaji elimu wataalam wa afya, Uongozi wa Halmashauri, pamoja na Kamati ya Huduma za



Scanned by CamScanner

Uchumi, Afya na Elimu na Vijana wa Chama cha Mapiduzi mnamo tarehe 22/04/2020 walifanya ziara ya kutembelea maeneo hayo kwa kutoa elimu ya ana kwa ana ikiambatana na utoaji wa ndoo 7 zenye ujazo wa lita 50 za kuwekea maji ya kunawia, pia wakawahimiza wananchi kutumia sabuni na vitakasa mikono katika maeneo hayo. Aidha, kamati ilipata maoni kutoka kwa wanananchi ambayo yanaendelea kufanyiwa kazi.

*Naomba kuwasilisha,*

John Paul Wanga
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**



Scanned by CamScanner